

## UANDISHI WA WASIA HALALI



Kijitabu hiki cha **Mahitaji ya Wasia Halali** ni dira ya kukusaidia kujua na kufahamu vyema namna ya kuandika wasia halali. Kijitabu hiki kitakuarifu kuhusu stakabadhi unazohitaji na utaratibu unaohitajika kufuata ili kuhakikisha kuwa wasia wako unatambuliwa kwa mujibu wa sheria

Uimarishaji Uwezo Kiasasi na KELIN Kenya

©2020 KELIN

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoweza kutoleshwa au kutumiwa katika umbo lolote lile au kwa njia nyingine bila kibali cha mchapishaji.



# MAHITAJI YA WASIA HALALI



## NINI MAANA YA WASIA?

Wasia ni tangazo la kisheria linalotolewa na mtu kuhusu heri zake kuhusiana na ugawaji mali yake baada ya yeye kuaga.

### AINA ZA WASIA:


Wasia unaweza kuandikwa au kusemwa.

### WATU WENYE UWEZO WA KUTENGENEZA WASIA:

- i. Mtu aliye na akili timamu
- ii. Mtu mzima (mtu wa umri zaidi ya miaka 18)

### MAHITAJI YA KIMSINGI YA WASIA ULIOANDIKWA:

- i. Uwe umeandikwa(kupigwa chapa au kuandikwa kwa kalamu).
- ii. Jina na anwani ya anayeandika wasia.
- iii. Umetiwa sahihi na kuandikwa tarehe na mwandishi wa wasia.
- iv. Kuwa na sahihi au alama ya kidole gumba ya mashahidi wawili waliohitimu (watu wazima wenye akili timamu)waliomwona mwandishi wa wasia akitia sahihi kwenye wasia (hasa mtu ambaye hanufaiki na wasia huo).



#### MAHITAJI YA KIMSINGI YA WASIA ULIOSEMWА:


- i. Kunenwa mbele ya mashahidi waliohitimu.
- ii. Mnenaji wa wasia kuaga katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kutengeneza wasia huo.

#### NAMNA YA KUHARIBU WASIA:

- i. Kuandika wasia mwингine au kiambatisho cha wasia (stakabadhi iliyoandikwa ya kurekebisha sehemu au wasia mzima).
- ii. Ndoa
- iii. Kuchoma hadi kuwa majivu.
- iv. Kutupa kama vile kutupa chooni au pahali ambapo hauwezi kupatikana.

#### PAHALI PA KUHIFADHIA WASIA:

- i. Benki
- ii. Ofisi ya wakili
- iii. Mmoja wa jamaa katika familia
- iv. Rafiki



#### SABABU ZA WASIA USIO HALALI:

- i. Ulaghai: uhalifu wa kudanganya ili kujinufaisha
- ii. Shurutisho: matumizi ya nguvu au vitisho
- iii. Uombaji: uombaji unaopita kiasi hadi kufikia kiwango cha kuudhi
- iv. Kosa
- v. Mgongano katika ushahidi wa mashahidi (hasa katika wasia wa kusemwa)

#### ATHARI YA UTOAJI ZAWADI KWA SHAHIDI KATIKA UTIAJI SAHIHI:

Inahitaji sahihi za watu wawili zaidi waliohitimu.

#### SEHEMU MUHIMU ZA WASIA:

- i. Ikirari/Ungamo
- ii. Batilisha kabla ya Wasia na Kiambatisho cha wasia
- iii. Uteuzi wa mtu atakayefaulisha matamanio yako (kabidhi wasii/msimamizi wa mirathi).
- iv. Uwezo wa msimamizi wa mirathi/wasii
- v. Jamaa katika familia
- vi. Urithi
- vii. Sahihi au alama ya kidole gumba ya mtengenezaji na mashahidi unapoandikwa.





### **OFISI YA NAIROBI**

Karen C, Njia ya Kuwinda,  
Kutoka Barabara ya Lang'ata  
S.L.P. 112 - 00202, KNH Nairobi  
Simu: 020 2515790  
Rununu: 0710 261408 / 0788 220300  
Kipepesi: 020 386 1390

### **OFISI YA KISUMU**

Mtaaa wa Nyalenda Railways,  
Bloku 9/220, Karibu na Barabara ya  
Nairobi, Mkabala wa YMCA  
S. L.P. 7708 - 40100 Kisumu - Kenya  
Simu: +254 57 204 1001